



MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR

**S.L.P. 3650
VICTORIA GARDEN
ZANZIBAR**

**SIMU: 024 223 2916
MOB: 0774 824242
FAX: 024 223 1461**

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA), inawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kutoa rushwa ya shilingi milioni 2.5 kwa mtendaji wa juu wa Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi.

Taarifa hiyo imetolewa na Kaimu Mkurugenzi wa Uchunguzi na Operesheni Nasir Ahmed Haji alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari Ofisini kwake Mnazimmoja wilaya ya Mjini Unguja.

Kaimu huyo alisema hayo kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa ZAECA alisema watu hao ni wafanyakazi wa kampuni ya IASIMJI ambao walitoa kiasi hicho cha fedha kwa mkurugenzi wa juu wa taasisi hiyo kwa lengo la kuruhusiwa ama kubadilishiwa majibu ya vipimo vya mchele.

Kaimu huyo alifahamisha kwamba bidhaa hiyo ilikuwa makontena 5 ikiwa sawa na tani 130 ambayo ilishafanyiwa uchunguzi na taasisi hiyo na kuonekana haufai kwa matumizi ya binadamu.

Akiwataja watu hao Kaimu huyo alisema ni pamoja na Imrani Amini Simji (34) mkaazi wa Mbweni Mkurugenzi mtendaji wa Kampuni ya IASIMJI Traders na

mtuhumiwa wa pili ni Moise Saifdin Muhsin (28) mkaazi wa Darajani ambae anajishughulisha na shughuli za clearing and fowering na mtuhumiwa wa tatu ni Raymond John Ribondo (31) mkaazi wa Kinondoni Dar Es Salaam ambae ni dereva wa taxi.

“Watu hao baada ya kupatiwa majibu hayo waliamua kufanya hivyo ili uonekane mchele huo unafaa kutumiwa na binadamu,” alisema.

Aidha alifahamisha kwamba uchunguzi zaidi juu ya watu hao unaendelea na utapokamilika watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Mbali na hayo alitumia fursa hiyo kuitaka jamii kushirikiana na serikali katika mapambano dhidi ya vitendo hivyo pamoja na kutoa taarifa pale wanapobaini kuna mwanya au harufu yoyote ya rushwa ili wahusika waweze kushughulikiwa.

Alifahamisha kwamba rushwa ni hatari na ina athaari kubwa kwa jamii hivyo mashirikiano ya pamoja baina ya serikali na wananchi ndio yatakayoweza kuzaa matunda ya kutokomeza vitendo hivyo.